



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb:HWR/K.2/VOL.IV/12/105

28/02/2022

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya

S.L.P 51

Ruangwa

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kwa mujibu wa kibali cha Ajira Mbadala chenye kumb.Na. FA.170/372/01 "A"/97 cha tarehe 31 Januari, 2022 kutoka kwa katibu Mkuu (UTUMISHI) Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenyewe sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi **Mtendaji wa kijiji Daraja la III** na **Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II**

❖ MTENDAJI WA KIJIZI DARAJA LA III-(NAFASI 2)

A. Sifa:

Mwomboji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au Sita (VI) aliyefaulu mafunzo ya Astashahada/Cheti" NTA Level 5" katika moja ya fani zifuatazo:-

Utarala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya jamii kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

B. KAZI NA MAJUKUMU YA AFISA MTENDAJI WA KIJIZI III

- 1) Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya
- 2) Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
- 3) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani, Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji.
- 4) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- 5) katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- 6) kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu

- 7) kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- 8) kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaaluma katika ngazi ya kijiji
- 9) kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Serikai ya kijiji
- 10) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika kijiji
- 11) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata
- 12) Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri

❖ **MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – (NAFASI 1)**

C. Sifa:

Mwomboji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au Sita (VI) aliyefaulu mafunzo ya NTA Level 5 Astashahada/Cheti cha utunzaji kumbukumbu katika moja wapo ya fani za afya ,masjala ,Mahakama na Ardhi.

D. KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II

Hili ni daraja la mafunzo katika kazi hivyo atafanya kazi kwa maelekezo ya Maafisa kumbukumbu walio juu yake kwa cheo. Kazi atakazojifunza na kufanya ni zile zifanywazo na Afisa kumbukumbu Daraja la I

E. NGAZI YA MSHAHARA

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kina ngazi ya Mshahara TGS B
Cheo cha Msaидizi wa kumbukubu Daraja la II kina ngazi ya Mshahara TGS. B

F. MASHARTI YA JUMLA


- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutumwa kwenye anwani iliyotajwa hapo chini.
- Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa, maelezo binafsi (CV) na nyaraka zote muhimu pamoja na picha mbili (2) (Passport size) zilizopigwa hivi karibuni.
- Testimonials “provisional results” “statement results’ hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (**FORM FOUR AND FORM SIX RESULTS SLEEPS) HAVITAKUBALIWA**

- Nafasi ya kazi iliyoombwa iandikwe juu ya bahasha, kutozingatia hii kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili
- Kwa wale watakaopita kwenye mchujo wa awali (short listened candidates). Ndio watakaoitwa kwenye usaili (interview) na kufika na vyeti halisi.
- Barua zote za maombi ziandikwe na kutumwa kwa njia ya posta kwa anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA,
S.L.P 51,
RUANGWA

**NB; Uwasilishaji wa barua za maombi kwa mkono katika ofisi
za Halmashauri ya Wilaya hazitapokelewa.**

**Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe 14 Machi,
2022 saa 9:30 Alasiri.**



George R. Mbesigwe
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

RUANGWA
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR,
RUANGWA DISTRICT COUNCIL
P. O. Box 51,
RUANGWA